

TAARIFA YA ENEO LA UWEKEZAJI WA VIWANDA KATIKA WILAYA YA MISUNGWI

1.0 UTANGULIIZI

Wilaya ya Misungwi imetenga eneo lenye ukubwa wa Hekta 2400 kwa ajili ya shughuli za uwekezaji katika kitongoji cha Nyang'olongo, eneo hili lipo ndani ya mipaka ya kata mbili za Bulemeji na Ukiriguru.

Eneo hili linatarajiwa kuendelezwa kwa kujengwa viwanda vikubwa hasa vya mazao ya kilimo kama, dengu, alizeti, pamba na mengineyo. Pia viwanda vya kusindika mazao ya mifugo kama nyama, ngozi na maziwa. Kwa vile wilaya ya Misungwi inapakana na ziwa Victoria inafikiria pia kuanzisha viwanda vya mazao ya uvuvi kama vile samaki.

2.0 LENGU

Lengu la kuanzisha uwekezaji huu ni kuinua uchumi wa wananchi wa Misungwi mmoja mmoja, wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla. Kwani uwekezaji huu utatoa ajira kwa wananchi na pia kuongeza pato la ndani na nje ya nchi.

Kwa vile eneo hili ni kubwa, Halmashauri ya wilaya itaandaa Master Plan ya eneo lote na kulipanga kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile viwanda, makazi ya umma na binafsi, huduma za kibiashara na huduma zingine za kijamii. Eneo hili linafaa kwa uwekezaji mkubwa kwani linafikika kwa urahisi, lipo kando kando ya barabara ya Mwanza-Shinyanga. Huduma ya umeme pia ipo karibu na eneo hili. Inakisiwa pia fidia ya ardhi katika eneo hili haitakuwa kubwa sana kulinganisha na maeneo mengine kwani eneo hili kwa asilimia kubwa linatumika kwa ajili ya shughuli za kilimo.

3.0 HALI HALISI YA ENEO KWA HIVI SASA

Eneo hili bado lipo chini ya umiliki wa wananchi wenyewe, kwa vile eneo ni kubwa utwaaji wake utakuwa wa awamu na utashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo ambao watakuwa tayari kulipa fidia na kuwekeza.

Tayari taarifa imetolewa kwa viongozi wa eneo hili wakiwamo madiwani na viongozi wa kata na vijiji. Aidha mpango huu ulisharidhiwa na kamati ya huduma za kiuchumi ya Halmashauri ya wilaya na Baraza la madiwani.

Hivi sasa taasisi mbili zimeonyesha nia ya kujenga vyuo vya elimu katika eneo hili taasisi hizo ni Chuo cha Biashara kinahitaji ekari 100 na chuo cha Mipango kina hitaji ekari 150, kwa vile eneo ni kubwa na Master Plan itakayoandaliwa itakidhi kwa mahitaji ya ardhi ya shughuli mbalimbali ni wazi kuwa eneo hili litakuwa kitovu kikubwa cha maendeleo kwa wilaya ya Misungwi.

3.0 SHUGHULI ZINAZOPASWA KUFANYIKA

Tayari mtaalam kutoka EPZA alikuja Misungwi 22/12/2016, alikagua eneo na kuonana na kutoa semina juu ya uwekezaji kwa wakuu wa Idara wa Halmashauri aliridhika na hatua ambayo tayali Halmashauri imefikia katika suala zima la maandalizi ya kutwaa eneo hili na alishauri hatua za utwaaji wa eneo kwa awamu uanze ikiwa ni pamoja na kuhamasisha jamii.

Shughuli ya kuhamasisha jamii katika eneo hili itanzaa karibuni ili zoezi la uthamini liweze kufanyika , na hatimaye ardhi iweze kutwaliwa kulingana na mahitaji ya viwanda, taasisi na wahitaji wengine wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Eneo hili litagawanywa katika blocks ndondogo zenye ukubwa wa kati ya Hekta mbili (2), tano (5) hadi hamsini (50) ili kuwezesha huduma na viwanda kujengwa kulingana na mahitaji halisi ya ardhi kwa shughuli husika.